JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

# TAARIFA KWA UMMA

## WATAHINIWA 7912 KUFANYA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE 2025 MANISPAA YA ILEMELA

Jumla ya watahiniwa **7912 (Wavulana 3801 na wasichana 4111)** waliosajiliwa kufanya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2025 katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela wameanza rasmi mtihani huo utakaofanyika kwa wiki mbili kuanzia tarehe **17 Novemba hadi 05 Disemba mwaka 2025.**

Kati ya watahiniwa **7912,** watahiniwa **7691** ni watahiniwa wa shule (**wavulana ni 3695** na **wasichana ni 3996)** na upande wa watahiniwa binafsi ni **221** (**wavulana wakiwa 106 na wasichana ni 115).**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, **Bi. Ummy Wayayu,** kwa niaba ya uongozi wa Ilemela anatoa rai kwa wazazi kuhakikisha wanawasimamia watoto wao ili waweze kufanya mitihani yao kikamilifu na amewaasa watahiniwa wote kuepukana na aina yoyote ya udanganyifu kwani wameandaliwa kikamilifu sambamba na kufuata taratibu, miongozo na sheria zote za mitihani.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ina jumla ya vituo **66** vya kufanyia mtihani, kati ya hivyo **vituo 55** vikiwa ni vituo vya shule na **vituo 11** ni vya watahiniwa binafsi.

Digitally Signed By Violencea S Mbakile
Mon Nov 17 10:16:47 EAT 2025

Violencea S Mbakile
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini